

**Usawiri wa Mwanamke na Mgawanyo wa majukumu kijinsia katika fasihi picha ya katuni
mnato za Kiswahili**

Elizabeth Nathaniel Chaligha

Digrii ya M.A. Kiswahili

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Institute of Kiswahili Studies, 2011.

Utafiti huu umejadiliwa kuhusu usawiri wa mwanamke na mgawanyo wa majukumu kijinsia katika fasihi picha ya katuni mnato za Kiswahili. Tatizo lililojenga utafiti huu ni kutokana na hali ya kila siku ya uchoraji wa katuni katika magazeti, majarida na katika wavuti ambazo humkweza mwanaume kinafasi na kimajukumu na kumshusha mwanamke, hivyo utafiti huu ulijikita kuchunguza nafasi ya mwanamke katika fasihi picha ya katuni mnato za Kiswahili. Utafiti huu ulitumia mbinu ya maktaba ni kwa kuchunguza katuni nyingi ilikupata ruwaza ya jumla kuhusu nafasi ya mwanamke na mgawanyo wa majukumu kijinsia. Pia umeongozwa na nadharia mbili- Nadharia ya Ufeministina Nadharia ya Ucheshi. Hivyo utafiti huu umebaini kuwa tofauti kubwa za kimajukumu kati ya mwanaume na mwanamke, kwani mwanamke amesawiriwa kwa mtazamo hasi yaani ameonekana ni kiumbe duni, mnyonge, na hivyo kuendelea kumdharau, kumkejeli na kumdhihaki. Hivyo basi kutokana na matokeo ya utafiti huu tumefikia mahitimisho kuwa katika jamii na fasi ya mwanamke na mgawanyo wa majukumu huwa tofauti na mwanaume kwasababu ya mila na tamaduni mbovu ambazo humchukulia mwanamke kama kiumbe duni wakati wote ingawa uhalisia wa sasa hauko hivyo. Utafiti huu umependekeza kuwa jamii inapaswa kumsawiri mwanamke kama kiumbe shupavu, mwanaye mtazamo wakuijenga na kuindele za jamii, kwahiyo kuwe na mgawanyo sawa wamajukumu. Mwisho utafiti umedokeza maeneo mengine ambayo yanatakiwa kufanyiwa utafiti zaidi; kumchambua mwanakatuni mmoja mmoja ilikujua falsafa yake katika fasihi picha ya katuni, na kutafiti vipengele vya fani na maudhui.